#tunawezesha

SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA

JARIDA LA DESEMBA

TOLEO LA 17

# WAZIRI MAKAMBA AAGIZA KUKAMILISHA KWA WAKATI MRADI WA UCHIMBAJI GESI ASILIA

**Dar es salaam,**

Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba, ameliagiza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) pamoja na Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), kuhakikisha mradi wa uchimbaji wa gesi asilia katika Kitalu cha Ruvuma kilichopo Mkoani Mtwara unakamilika kwa wakati...

» UK.1




Waziri wa Nishati **Mhe. January Makamba**, Mkurugenzi Mtendaji (TPDC) **Dkt. James Mataragio** Mwenyekiti wa Aminex na Ndovu Resource **Ndg.Charles Santos** na Mkurugenzi wa ARA Petroleum (Tanzania) **Ndg.Erhan Saygi** baada ya kusaini Mkataba wa Nyongeza wa Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (PSA) Kitalu cha Ruvuma-Mtwara

## TPDC YAENDESHA ZOEZI LA UTOAJI ELIMU YA MIUNDOMBINU YA GESI ASILIA MKOANI LINDI

» UK.2

## KYOBA AAGIZA VIONGOZI WA KATA KUSIMAMIA KIKAMILIFU ZOEZI LA FIDIA BOMBA LA GESI

» UK.5



## Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

# TAHARIRI

## Mradi wa EACOP Kukuza Uchumi wa Nchi

Maendeleo ya nchi yoyote yanategemea sana ukuaji wa Sekta mtambuka ya nishati ambapo uwepo wa nishati na miundombinu ya uhakika inaongeza chachu ya ukuaji wa uchumi wa nchi na maendeleo ya mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Serikali ya Tanzania kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) imekuwa mstari wa mbele katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati ukiwemo mradi wa ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Hoima -Uganda hadi Chongoleani -Tanga lenye urefu wa kilometa 1443 ambapo mradi huu utagharimu kiasi cha shilingi Trillioni 8 za Kitanzania mpaka kukamilika kwake.

Mradi huu utawezesha mafuta yaliyopatikana nchini Uganda kusafirishwa kwenda kuuzwa katika masoko ya Kimataifa. Utekelezaji wa mradi, ulianza kwa kusaini mkataba wa awali wa makubaliano kati ya Uganda na Tanzania (Intergovernmental Agreement - IGA) ambao ulifuatiwa na Mkataba wa Nchi Hodhi (Host Government Agreements – HGA) kati ya mwekezaji (EACOP) na nchi husika. Aidha maamuzi ya mwisho ya uwekezaji (Final Investment Decision) yalifanyika tarehe 01 Februari 2022 nchini Uganda na hivyo kuruhusu rasmi kuanza kwa utekelezaji wa mradi.

Utekelezaji wa mradi uko katika hatua nzuri ambapo utwaaji wa maeneo ya awali umeshakamilika kwa asilimia 100%. Maeneo hayo ni yale ambayo vituo vya kusukuma mafuta (pump station), makazi ya wafanyakazi kipindi cha ujenzi, maeneo ya kuhifadhi mabomba pamoja na eneo la kuandaa mabomba vitajengwa. Aidha, utoaji wa elimu kwa wananchi 9,516 watakaopitiwa na mradi ni zoezi endelevu ambalo linahusisha kutoa elimu kuhusu stahiki kwa mujibu wa sheria katika utwaaji ardhi, elimu ya fedha na uwekezaji pamoja na elimu ya kilimo cha kisasa.

Vilevile, utekelezaji wa mradi huu unazingatia sheria za nchi pia sheria za Kimataifa ambapo wananchi waliopoteza makazi wanapata fursa ya kuchagua kujengewa nyumba za kisasa au kulipwa pesa pekee na jumla ya nyumba 309 zinaendelea kujengwa. Hakika uwepo wa mradi wa EACOP utanufaisha nchi zote mbili kwa kufungua fursa za maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wakati wa matayarisho ya ujenzi,wakati wa ujenzi na wakati wa uendeshaji wa mradi.

Kwa upande wa Tanzania, bomba hili linapita katika Mikoa 8 ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga. Mradi huu utaiWletea nchi ya Tanzania manufaa kadha wa kadha yakiwemo ya kuongezeka kwa uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni nchini, ongezeko la mapato ya Serikali, ajira, ukuaji wa sekta ya biashara na usafirishaji, uboreshwaji wa baadhi ya miundombinu pamoja na kuchochea na kuvutia wawekezaji wa kigeni chini.

# WAZIRI MAKAMBA AAGIZA KUKAMILISHA KWA WAKATI MRADI WA UCHIMBAJI GESI ASILIA




**Dar es salaam,**

Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba, ameliagiza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) pamoja na Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), kuhakikisha mradi wa uchimbaji wa gesi asilia katika Kitalu cha Ruvuma kilichopo Mkoani Mtwara unakamilika kwa wakati.

Mhe. Makamba aliyasema hayo tarehe 25/11/2022 Jijini Dar es Salaam wakati wa halfa ya uwekaji saini Mkataba wa Nyongeza wa Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (PSA) Kitalu cha Ruvuma-Mtwara kati ya Wizara ya Nishati, TPDC, Kampuni ya ARA Petroleum na Kampuni ya Ndovu Resources.

"Dhamira ya Serikali ni kuona mradi huo unakamilika ndani ya miezi 12 hadi 18 na hatutegemei kusikia mradi huo unachelewa kutokana na changamoto ya fedha.Mradi huo ukikamilika utakuwa mradi wa kwanza wa gesi ambao utalinufaisha Taifa katika nyanja mbalimbali ikiwemo Serikali kupata Mrahaba (12.5%), kupata kodi, Serikali kupata gawio la mapato yatokanayo na mauzo ya gesi pia ajira kwa Wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara" alisema Mhe. Makamba.

Dkt. Mataragio alisema kuwa uwekezaji huo wenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 500 unatarajiwa kuzalisha takribani futi za ujazo trilioni 1.6 ambacho ni kiasi cha gesi kilichogunduliwa katika eneo hilo na kuweka wazi kuwa utekelezaji wake utasaidia kuongeza chachu na wawekezaji wengi zaidi.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya ARA Petroleum (Tanzania) Ndg. Erhan Saygi ameishukuru Serikali ya Tanzania hususan Viongozi wa Serikali za Vijiji kwa ushirikiano waliouonyesha na kuongeza kuwa kukamilika kwa mradi kutachagiza uboreshaji wa miundombinu na kuongeza ajira ili kukuza pato la wananchi na Taifa kwa ujumla.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Viongozi mbalimbali akiwemo Mkuu wa Mkoa wa Lindi Bi. Zainab Telack, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Kanali Ahmed Abbas Ahmed pamoja na Wabunge wa Mikoa ya Lindi na Mtwara.




*Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba, Mkurugenzi Mtendaji (TPDC) Dkt. James Mataragio Mwenyekiti wa Aminex na Ndovu Resource Ndg.Charles Santos na Mkurugenzi wa ARA Petroleum (Tanzania) Ndg.Erhan Saygi wakisaini Mkataba wa Nyongeza wa Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (PSA) Kitalu cha Ruvuma-Mtwara*

# TPDC YAENDESHA ZOEZI LA UTOAJI ELIMU YA MIUNDOMBINU YA GESI ASILIA MKOANI LINDI

**Lindi,**
Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) liliendesha zoezi la utoaji elimu kwa Wananchi wa Vijiji/Mitaa inayopitiwa na miundombinu ya gesi asilia.Shirika limekua na utaratibu wa kutoa elimu kwa umma juu ya miradi mbalimbali ya utafiti na uendelezaji wa nishati ya mafuta na gesi asilia nchini. Elimu hii imetolewa ikiwa ni sehemu ya kuimarisha mahusiano mazuri na kuwajengea uwezo wananchi kutambua fursa za uwekezaji wa miradi ya gesi pamoja na kuimarisha ulinzi na usalama wa miundombinu ya bomba la gesi asilia.

Zoezi hilo lilifanyika Mkoani Lindi kupitia mikutano ya hadhara katika Vijiji ambavyo vimepitiwa na mradi wa bomba la gesi asilia ambapo elimu hiyo ilijikita kwenye mada za ulinzi na usalama, fursa zinazoambatana na miradi ya gesi asilia (manufaa) pamoja na Uwajibikaji wa Shirika kwa Jamii (CSR).

Akizungumza katika moja ya mikutano na wananchi wa Kijiji cha Somanga Kusini, Afisa Maendeleo ya Jamii wa TPDC Bw. Oscar Mwakasege alieleza kuwa utunzaji na usalama wa mradi wa bomba la gesi asilia nchini ni pamoja na ushirikishwaji wa wananchi katika ngazi zote hususani katika kupata taarifa, elimu, utekelezaji wa miradi ya kijamii pamoja na ushirikishwaji kwenye ulinzi na usalama.




"Mradi wa bomba la gesi asilia umekua na manufaa makubwa kwa jamii na Taifa kwa ujumla ambapo mpaka sasa 70% ya umeme nchini unazalishwa kwa kutumia gesi asilia hivyo kuchagiza ukuaji wa Sekta mbalimbali, kadhalika gesi asilia inatumika kuendeshea mitambo viwandani ambapo viwanda vipatavyo 53 na nyumba takribani 1500 za Mikoa ya Dar es salaam, Mtwara na Lindi (Mnazi mmoja) zimeunganishwa katika mtandao wa gesi asilia kwa matumizi ya kupikia majumbani, aidha mpaka sasa zaidi ya magari 1500 yanatumia gesi asilia kama nishati mbadala wa petroli na dizeli,"alisema Mwakasege.

Katika hatua nyingine Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Usalama TPDC Bw.Fredy Mfikwa alieleza kuwa mradi wa bomba la gesi asilia umegusa Vijiji na Mitaa 139 kuanzia Msimbati Mtwara hadi Dar es salaam. Aidha, alieleza kuwa TPDC inashirikiana vizuri na Vijiji/Mitaa hiyo kwenye suala la ulinzi na usalama ikiwa ni - pamoja na kutoa fedha kila mwezi kwa kila Kijiji/Mtaa ili kuwezesha vijiji hivyo kufanya usafi kwenye njia (Mkuza) wa bomba la gesi asilia.

Bw.Mfikwa alitoa rai kwa wananchi kuendelea kuitunza miundombinu ya bomba la gesi asilia kwa kuacha kufanya shughuli hatarishi za kibinadamu ndani ya miundiombinu hiyo, pamoja na kuwasisitiza wananchi kuendelea kutoa taarifa kwa uongozi wa Vijiji/Mitaa au TPDC pindi wanapoona mazingira hatarishi ndani ya miundombinu ya bomba la gesi asilia.

"Shughuli za kibinadamu ambazo hazipaswi kufanywa ndani ya Mkuza wa bomba la gesi asilia kama kuchimba mchanga, kilimo cha mazao ya muda mfupi na mrefu, kuchoma nyasi moto, kupitisha makundi makubwa ya mifugo na shughuli zozote za ujenzi haiziruhusiwi, hivyo natoa rai kwa Uongozi wa Vijiji na wananchi kuendelea kudumisha ulinzi na usalama ili bomba hilo liendelee kuwa na manufaa kwa sasa na baadae," alieleza Mfikwa.

# TPDC IMETOA JUMLA YA SHILINGI 1.5 BILIONI KWENYE SHUGHULI ZA KIJAMII NCHINI




**Lindi,**
Hayo yamezungumzwa na Kaimu Meneja wa Kitengo cha Usalama cha GASCO kampuni tanzu ya TPDC ndugu Fred Mfikwa wakati akikabidhi viti na meza 85 kwa Shule ya Sekondari ya Kikanda Mkoani Lindi.

"Uwajibikaji kwa jamii ni kipaumbele cha Shirika ikiwa mpaka sasa zaidi ya shilingi bilioni 1.5 zimetumika kutekeleza miradi mbalimbali ya kuinua huduma za kijamii kwenye maeneo ambayo miradi ya gesi asilia inatekelezwa", ameeleza ndugu Mfikwa.

Mfikwa amebainisha kuwa, kwa kiasi kikubwa Shirika limekuwa likichangia katika nyanja kuu nne ambazo ni sekta ya afya, maji, elimu pamoja na utawala bora, hayo ni maeneo ambayo yanagusa moja kwa moja maisha ya kila siku ya wananchi

Ndugu Mfikwa amongeza kuwa kwa upande wa Mkoa wa Lindi TPDC imetekeleza ujenzi wa miradi ya maji ikiwemo mradi wa maji katika Kijiji cha Songosongo na Kilangala B, ujenzi wa matundu ya vyoo katika shule, ujenzi wa madarasa, ujenzi wa maabara shuleni, kudhamini michezo pamoja na ujenzi wa majengo ya ofisi za Serikali za Mitaa na Vijiji.

Aidha kwa upande wake Afisa Maendeleo ya Jamii wa TPDC Bi. Kwigema Anthony akiongea katika hafla ya kukabidhi samani hizo amesema kuwa kilichofanyika ni muendelezo wa jitihada za TPDC katika kuboresha huduma mbalimbali za kijamii kama vile afya, maji, utawala bora na hili la elimu nchini.

Wakizungumza baada ya kukabidhiwa samani baadhi ya Walimu, Viongozi wa Kata na Wanafunzi wameishukuru TPDC kwa kuwapatia samani na kueleza kuwa samani hizo zitawasaidia wanafunzi kujifunza kwa ufanisi mkubwa na vitapunguza changamoto ya viti na meza ambayo ilikuwepo hapo awali.

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limekuwa likitekeleza Sera ya Shirika ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) ya mwaka 2017, lengo likiwa ni kuendelea kudumisha uhusiano kati ya Shirika na jamii zinazoguswa na miradi ya mafuta na gesi asilia pamoja na maendeo mengine nchini.

# GESI ASILIA KUKUZA SEKTA YA VIWANDA




Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kutoka TPDC Bi. Marie Msellemu akitoa maelezo kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt. Jim Yonazi kuhusu manufaa ya matumizi ya gesi asilia kwa Nchi

**Dar es Salaam,**

Hayo yamezunguzwa na Meneja Mawasiliano wa TPDC Bi. Marie Msellemu katika Maonesho ya Saba ya Viwanda yenye kauli mbiu ''Nunua Bidhaa za Tanzania Jenga Tanzania" yaliyofanyika tarehe 4-9 Desemba 2022 katika Viwanja vya Mwl. J.K Nyerere Jijini Dar es salaam.

"Lengo la TPDC ni kuongeza matumizi ya gesi asilia nchini yakiwemo ya viwandani ili kukuza ukuaji wa viwanda nchini, kwenye magari na kupikia majumbani kwakuwa gesi hii ina ufanisi, safi na nafuu ukilinganisha na vyanzo vingine vya nishati kama mafuta, mkaa na kuni."

Bi. Msellemu amesema kuwa mpaka sasa zaidi ya viwanda 53, magari 1500 na nyumba takribani 1500 zimeshaunganishwa na mtandao wa gesi asilia katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es salaam. "TPDC ni mdau mkubwa katika Sekta ya viwanda na ndio maana tumeshiriki katika maonyesho hayo ili kuweza kubaini changamoto mbalimbali kutoka kwa wadau wa viwanda ili zitusaidie kuboresha huduma zetu pia kupokea pongezi kwa maeneo yanayofanya vizuri."

Aidha, Bi. Msellemu alisema gesi asilia ina mchango mkubwa katika kuzalisha umeme nchini ambapo mpaka sasa zaidi ya asilimia 60 ya gesi asilia inatumika kuzalisha umeme.

Halikadhalika, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt. Jim Yonazi aliwapongeza TPDC kwa kuanzisha mfumo wa gesi asilia wenye gharama nafuu kwa wananchi. Pia amewaomba kuongeza kasi ya ujenzi wa miradi ya usambazaji gesi asilia kwa Mikoa yote Nchini.

# KYOBA AAGIZA VIONGOZI WA KATA KUSIMAMIA KIKAMILIFU ZOEZI LA FIDIA BOMBA LA GESI



*Wananchi wa Vijiji vinavyopitiwa na bomba la gesi asilia kutoka Ntorya hadi Madimba wakiwa katika mkutano wa hadhara ulioandaliwa na TPDC kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mtwara kwaajili ya kuhakiki taarifa za malipo ya fidia kupisha ujenzi wa bomba la gesi asilia*

**Mtwara,**
Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Mhe. Dastan Kyobya ametoa maagizo hayo wakati wa ufunguzi wa zoezi la uhakiki wa wananchi waliofanyiwa uthamini wa maeneo yao ili kupisha utekelezaji wa Mradi wa bomba la gesi lenye urefu wa kilomita 35 kutoka Ntorya (Kisimani) hadi Madimba kwenye kiwanda cha kuchakata gesi asilia ambapo jumla ya wananchi 253 watalipwa fidia.

''Niwaombe Viongozi wa Kata zote zinazopitiwa na bomba mhakikishe mnasimamia zoezi hilo vizuri, pitieni taarifa zao jina kwa jina, mtu kwa mtu na sura kwa sura ili baada ya malipo kusiwepo na changamoto ya malalamiko kutoka kwa wahusika halali,'' alisema Kyobya.

Aidha, Diwani wa Kata ya Nanguruwe.Mhe. Patrick Wayziman Simwinga aliipongeza TPDC kwa kuendesha zoezi la uthamini na uhakiki wa mali za wananchi wa maeneo yanayopitiwa na mkuza wa bomba kwa uwazi na ikiwemo kufanya mikutano ya hadhara kwa ajili ya kutoa elimu ya awali ya uthamini wa mali za wananchi ikiwemo ardhi, nyumba, mashamba na mazao.

"Naipongeza TPDC kwa kuendesha zoezi hilo limesaidia kuondoa migogoro baina ya wananchi ambao wanahusika na Mradi huu kwani migogoro hiyo isingetatuliwa katika hatua za awali kama mlivyofanya TPDC ingesababisha kukwamisha utekelezaji wa Mradi. Pia niwaombe TPDC malipo hayo ya fidia yafanyike kwa wakati ili Wananchi waliopisha Mradi huo waweze kutafuta maeneo mengine ya kufanya shughuli zao za kiuchumi," alisema Simwinga.

Nae Afisa Miliki Mwandamizi kutoka TPDC Bi. Happy Mwaseba alisema Mradi wa bomba la gesi asilia kutoka Ntorya hadi Madimba unatarajia kutoa fursa mbalimbali za kiuchumi ikiwa ni pamoja na ajira za muda mfupi kwa wananchi katika vijiji ambavyo vimepitiwa na bomba hilo katika kipindi cha utekelezaji wa Mradi ikiwemo fursa ya kutoa huduma mbalimbali kwa wafanyakazi wataohusika katika shughuli za ujenzi huo.

Mradi wa bomba la gesi asilia lenye urefu wa kilometa 35 kutoka Ntorya hadi Madimba na kugusa kata 5 na vjiji 13 ndani ya Tarafa ya Ziwani iliyoko Wilaya ya Mtwara unategemewa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 70.

# WANANCHI WASISITIZWA KULINDA MIUNDOMBINU YA GESI ASILIA

**Mtwara,**

Rai hii imetolewa na Bw. Elias Muganda  Afisa Usalama toka GASCO Kampuni Tanzu ya TPDC wakati wa utekelezaji wa pamoja wa zoezi la kutoa elimu ya usalama wa miundombinu ya gesi asilia kwa wananchi wanaozunguka miundombinu ya gesi asilia katika Mkoa wa Mtwara. ”Kulinda na kutunza miundombinu ya gesi asilia kwenye maeneo yenu ni sehemu ya kutimiza jukumu la msingi la kutunza rasilimali za nchi kwa maendeleo ya Taifa”.

“TPDC inawasisitiza Wananchi wote kuendelea kushirikiana na Serikali katika jukumu la kulinda miundombinu ya gesi asilia kwa sababu miradi hiyo ni kipaumbele cha uchumi wa Taifa letu kwa kiasi kikubwa hivyo kila Mwananchi anajukumu la kuhakikisha miundombinu hii inakuwa salama wakati wote,” alisema Muganda.

Katika hatua nyingine, Afisa Maendeleo ya Jamii kutoka TPDC Bw. Ally Mluge aliwaeleza Wananchi umuhimu na faida za matumizi ya gesi asilia katika kukuza uchumi wa Taifa ikiwemo, uzalishaji wa umeme, uendelezaji wa viwanda mbalimbali, matumizi ya gesi kupikia majumbani pamoja na kuendeshea magari.

Diwani wa Kata ya Msimbati Mhe. Rashid Lincon ameishukuru TPDC kwa kuendesha zoezi hilo la uelimishaji jamii na kusema kwamba, zoezi hilo limesaidia kuongeza uelewa wa masuala yanayohusiana na gesi asilia pamoja na faida zake. Vilevile ameiomba TPDC kutoa elimu mara kwa mara kwa Wananchi ili waweze kufahamu zaidi juu ya miradi inayotekelezwa na Serikali. “Tunawashukuru sana TPDC kwani elimu hii itasaidia katika kufahamu namna sahihi ya kutumia gesi asilia na pia kuepuka hatari ambazo zinaweza kujitokeza pindi kunapotokea hitilafu ya kuvuja kwa gesi asilia.”

Mbali na elimu hiyo inayotolewa na TPDC kuhusiana na usalama wa miundombinu na watumiaji wake, Shirika limekuwa mdau mkubwa wa maendeleo ya Mtwara ambapo mara kadhaa imekuwa ikishiriki vyema katika shughuli za kijamii kupitia Sera ya uwajibikaji kwa jamii. TPDC imekuwa ikichangia zaidi katika kuimarisha Sekta za afya, maji, elimu pamoja na utawala bora.


Afisa Usalama Mwandamizi kutoka Kampuni Tanzu ya GASCO Bw.Elias Muganda akitoa elimu kuhusu ulinzi na usalama wa miundombinu ya gesi asilia kwa wananchi wanaoishi jirani na miundombinu katika Kijiji cha Mgoji Mkoani Mtwara

# TPDC YAENDESHA SEMINA KWA WAANDISHI WA HABARI

**Morogoro,**

Waandishi wa Habari wamekumbushwa kutumia vyema taaluma yao kuisemea Sekta ya mafuta na gesi asilia nchini ambayo imekuwa na mchango mkubwa katika Uchumi wa Taifa.

Hayo yamesemwa na Meya wa Manispaa ya Morogoro Mhe. Paschal Kihangi wakati wa ufunguzi wa semina ya Waandishi wa Habari kuhusu Sekta ya mafuta na gesi asilia Mkoani Morogoro.

Semina hiyo imeandaliwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ikiwa na lengo la kuwajengena uwezo wa kujua Miradi ya kimakakati inayosimamiwa na Shirika hilo.

Akizungumza wakati wa semina hiyo Mhe. Kihangi amesema Waandishi wa Habari ni kundi muhimu nchini na kupitia wao wananchi wanapata taarifa sahihi kwa wakati kuhusu fursa mbalimbali na kuelewa Miradi ya utafutaji na uendeshaji wa rasilimali ya mafuta na gesi.

Aidha, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kutoka TPDC Bi. Marie Msellemu, alisema kufanyika kwa semina hiyo mkoani Morogoro ni muendelezo wa semina mbalimbali ambazo zimekuwa zikitolewa kwa Wadau nchini ili kuwajengea uwezo wa kujua Miradi ya kimakakati kwa nchi hasa iliyopo chini ya TPDC.

Serikali inaendelea kutekeleza Miradi 19 ya kimkakati huku Miradi 9 ikiwa Wizara ya Nishati na Miradi 4 ikisimamiwa na TPDC.

Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa kusindika gesi asilia kuwa kimiminika (LNG), Mradi bomba la kusafirisha mafuta ghafi Afrika Mashariki (EACOP), mradi wa utafutaji wa mafuta Bonde la Eyasi Wembere pamoja na Mradi wa utafutaji wa gesi asilia Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini.



*Meya wa Manispaa ya Morogoro Mhe. Paschal Kihangi (wa pili kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Waandishi wa Habari walioshiriki semina ya kuwajengea uwezo wa kutoa taarifa sahihi kuhusu sekta ya mafuta na gesi asilia Nchini*

# HABARI PICHA



**Jarida la Disemba**
**TOLEO 17**
**2022**






Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba, Mkurugenzi Mtendaji (TPDC) Dkt. James Mataragio Mwenyekiti wa Aminex na Ndovu Resource Ndg.Charles Santos na Mkurugenzi wa ARA Petroleum (Tanzania) Ndg.Erhan Saygi wakisaini Mkataba wa Nyongeza wa Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (PSA) Kitalu cha Ruvuma-Mtwara




Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar Mhe. Omar Said Shaaban (wa pili kushoto) akipewa maelezo na Mhandisi Eva Swillah kutoka TPDC kuhusu namna gesi asilia inavyosafirishwa kutoka kwenye visima vya gesi Msimbati kwenda Kiwanda cha Kuchakata gesi Madimba hadi kuwafikia wateja kwa wa viwandani, majumbani na kwenye magari kwa ajili ya matumizi



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya Dkt. Rashid M.Chuachua (mwenye tai nyekundu) akiwa katika picha ya pamoja na Waandishi wa Habari wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wakati wa ufunguzi wa warsha ya kuwajengea uwezo wa kutoa taarifa sahihi kuhusu sekta ya mafuta na gesi asilia

## TPDC-Mini Marathon-Mtwara na Lindi












## TPDC-Mini Marathon-Mtwara na Lindi







# BODI YA WAHARIRI

**MHARIRI MKUU**

Marie Msellemu

**WAJUMBE**

Malik Munis
Beatrice Peter
Oscar Mwakasege
Delian Kabwogi
Ally Mluge
Kwigema Anthony
Eugene Isaya
Jacobo Haule



**LIMETOLEWA NA:**

Kitengo cha Mawasiliano
Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)
Benjamin W. Mkapa Pensions
Towers, Azikiwe/Jamuhuri Street
S.L.P. 2774, Dar Es Salaam, Tanzania
Simu:+255 22 2200103/4, 2200112.
Nukushi: +255 22 22 2200113
Barua pepe: info@tpdc.co.tz
Tovuti: www.tpdc.co.tz



# JARIDA LA TPDC

## TOLEO LA 17

2022